JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MEI NA JUNI, 2025

### 1.0 UTANGULIZI


Katika kipindi cha mwezi ya Mei, 2025 mvua ziliendelea katika baadhi ya maeneo nchini, sambamba na ongezeko kidogo la mvua katika hususan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hali hii ilisababisha ongezeko la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa baadhi ya maeneo. Aidha, lakini pia ilisababisha mafuriko na kutuama kwa maji katika maeneo mengine. Kwa mwezi Juni 2023 baadhi ya maeneo yalipata vipindi vya upepo mkali pamoja na hali ya baridi, ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe 2025. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa za mwelekeo wa hali ya hewa za misimu zilizotolewa hapo awali.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Mei, 2025

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa pamoja na ngurumo vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali, na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 101.0 kwa saa 24 kilirekodiwa Zanzibar mnamo tarehe 1 Mei, ikifuatiwa na milimita 84.6 katika kituo cha Lyamungu mnamo tarehe 5 Mei na milimita 84.4 katika kituo cha Bukoba mnamo tarehe 13 Mei, 2025. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa  kwa mwezi Mei, 2025.

Kutokana na mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha, taarifa kutoka katika vyombo vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari mbalimbali katika baadhi ya maeneo nchini. Athari hizo ni pamoja na uharibifu wa mali na miundombinu ambayo inaweza kuhatarisha maisha ya watu.



**Kielelezo 2**: Wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoa wa Kilimanjaro wakiondoa magogo katikati ya Barabara Kuu ya Dar es salaam – Moshi - Arusha, eneo la Kiboriloni Manispaa ya Moshi Mkoani Kilimanjaro mnamo tarehe 6 Mei, 2025. (Chanzo: *Gazeti la Mwananchi*)..

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**1.2 Hali joto kwa mwezi Mei, 2025**

Katika kipindi cha mwezi Mei 2025, hakuna ripoti ya vipindi vya joto kali vilivyorekodiwa nchini. Aidha, kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 32.7 °C kilirekodiwa katika kituo cha Dar es Salaam mnamo tarehe 22 Mei 2025..

Kwa upande mwingine, hali ya baridi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 8.1 °C kilirekodiwa katika kituo cha Uyole mnamo tarehe 25 Mei 2025. Kaika kipindi cha mwezi mzima, Kituo cha Uyole kilirekodi viwango vya nyuzi joto 10 au chini kwa siku kumi na nne (14) wakati kituo cha Igeri kilireekodi hali hiyo kwa siku tisa (9).

**1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Mei, 2025**

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani (ikihusisha mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara na visiwa vya Unguja na Pemba), kati mwa nchi (Singida na Dodoma) na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Iringa na Songwe).

Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa vumbi na kupeperushwa kwa takataka na kusababisha kupungua kwa uono na kuathiri ubora wa hewa angani. Maeneo ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao wa pwani.

**1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Juni, 2025**

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2025 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan maeneo ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki.. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilirekodiwa. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 97.2 kilirekodiwa katika kituo cha Matangatuani mnamo tarehe 8 Juni, ikifuatiwa na milimita 65.8 katika kituo cha Pemba mnamo tarehe 10 Juni 2025. Aidha, kituo cha JNIA kilirekodi milimita 57.5 na Kituo cha Pemba milimita 51 mnamo tarehe 8 Juni 2025.

**1.5 Hali joto kwa mwezi Juni, 2025**


Katika kipindi cha mwezi Juni 2025, hakuna vipindi vya joto kali vilivyoripotiwa nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 31.8 °C kilirikodiwa katika kituo kilichopo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere (JNIA) mnamo tarehe 2 na 3 Juni, 2025. Kwa upande mwingine, hali ya baridi kali ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 6.6 °C kilirekodiwa katika kituo cha Igeri mnamo tarehe 23 na 29 Mei 2025. Jedwali

namba 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo kituo kimerekodi kiwango cha joto la chini cha nyuzi joto 10 °C au chini ya  nyuzi joto 10 °C.

Jedwali 1. Idadi ya siku ambazo vituo vilirekodi viwango vya joto la chini vya nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 katika mwezi Juni, 2023

| Kanda | Kituo | Idadi ya Siku (≤ 10 °C) | Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa ($^{0}$C) |
|---|---|---|---|
| **Southwestern highlands** | Uyole | 25 | 7.0 °C |
| | Igeri | 26 | 6.6 °C |
| | Mbozi | 12 | 7.8 °C |
| | Sumbawanga | 6 | 9.6 °C |

Kielelezo cha 3 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku kwa mwezi Juni, 2024 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi kali ilianza kujitokeza katika wiki ya kwanza mwezi Juni, ikifuatiwa na ongezeko kidogo la joto kuelekea mwishoni mwa wiki ya kwanza. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya Uyole  ukilinganisha na kituo cha Igeri.




Kielelzo 3. Viwango vya joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi June, 2024.

### 1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Juni, 2025

Kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini ilipelekea kutokea kwa vipindi vya upepo mkali wa kusi unaofikia au kuzidi kilomita 40 katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani,

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), kati mwa nchi (Singida), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) na maziwa makuu. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 10 Julai, 2025*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz